

TIST

HABARI MOTO MOTO®

Tel. 026-2322246, P.O.BOX 53 MPWAPWA

E-Mail tist@twiga.com

January 2002

Starting the New Cash for Trees Program

TIST is beginning the new program to help small groups! TIST will make quarterly payments to groups for each member trees and seedlings. Groups heard about this in the Deanery meetings and the last HMM. Here is more information.

TIST Will Count Trees and Make Payments

TIST groups can qualify if they have 1 acre of conservation farming acres per member, have planted 2000 trees (1000 for new groups) and each member signed the application and covenant.

Quantifiers will visit all groups 4 times per year, or one time every 3 months. Quantifiers will visit each grove and count all living trees. They also will count all living seedlings in nurseries.

Quantifiers will then share the total number of trees

Mambo muhimu ya kukumbushana.

- Hakikisha umeshapanda miti yako kabla ya msimu wa mvua kwisha.
- Kumbuka kutoa viriba kabla ya kupanda mti wako kwenye shimo, kwani ukipanda na viriba, vitazuia mizizi isipenye kwenye udongo.
- Kumbuka kuweka kumbukumbu ya idadi ya watu waliotumia kilimo hai kwenye kikundichako, ili tuweze kupata taarifa kwa usahihi bila kusahau ukubwa wa shamba.
- Hakikisha kuwa umetoa / umeondoa viriba kabla ya kupandikiza miche yako.
- Tuma taarifa za Mwezi kupitia Quantifaya wanaohudhuria mikutano ya Parishini.

Kuanza malipo mapya ya fedha katika upandaji miti.



Conservation farming in Chamkoloma Parish

TIST imeanzisha mpango mpya kwa ajili ya kuvisaidia vikundi vidogovidogo.

TIST itatoa robo ya malipo kwa vikundi kwa ajili ya miti na mbegu. Vikundi vilijulishwa suala hili katika mikutano ya Dinari na katika HMM ya mwisho. Na hii ni taarifa zaidi.

TIST itahesabu miti na kuifanyia malipo.

Vikundi vya TIST vitafuzu ikiwa vitakuwa na hekari 1 ya kilimo hai kwa kila mshiriki, iwapo kikundi kimekwishapanda miti 2000 (miti 1000 kwa kikundi kipya) na kusaini makubaliano ya kwenye maombi.

Kwantifaya watatembelea vikundi mara nne kwa mwaka, au mara moja kila baada ya miezi mitatu. Pia kwantifaya watatembelea kila shamba la miti (grove) na kuhesabu miti yote iliyo hai, vilevile watahesabu miche yote katika vitalu.

Kwantifaya watashirikiana na mwakilishi wa kikundi kuhusiana na jumla ya idadi ya miti na miche waliohesabu. Kwantifaya watamwomba muwakilishi kuweka sahihi katika fomu kulingana na idadi iliyohesabiwa.

Continued on page 2

and seedlings they count with a group representative. Quantifiers will ask the representative to sign a form with the total number counted.

Quantifiers will bring that number back to the TIST office. TIST staff will multiply the number of trees and seedlings by the 4/- payment, and prepare a report for the group to send back with quantifiers. Many small groups are still paying back loans from last year. TIST will put their quarterly tree payments into an account to reduce the remaining loan. When the loan is paid, the group can receive cash.

Groups that repaid loans can receive new cash. TIST will put their payment into an account. TIST will report to groups how much cash is in the account. Groups can ask quantifiers to bring the cash when they return the following month.

Here are three ideas to help your group:

- Pay back loans quickly so your group can get new cash.
- Plant more trees now to pay back soon and have more cash later.
- Leave cash in the account with TIST so that it can grow over time. The group can then buy larger items like a bicycle or improved grain, at a later date.

Regular Meetings at Parishes

Parishes are being asked to hold meetings of all small group members one time per month. Quantifiers or TIST staff will attend these meetings. All small group members should come to these meetings. At this monthly parish meeting, small group members will:

- Receive an account statement of how much money is in their account
- Receive money they have requested
- Receive the new Habari Moto Moto
- Give the Small Group Monthly Report about the small group meetings to Quantifiers
- Discuss questions about the program
- Share good news from small group work.
- Share njia bora

Groups must give Small Group Monthly Reports to TIST to keep getting tree payments. These reports are used to help TIST and the dmp know how best to serve the small groups and what training is needed for small groups.

TIST is working very hard to help the small groups. Please be patient as TIST learns to do this new program in the most careful and accurate way to help the most groups.

Kwantifaya watawasilisha idadi hiyo ya miti katika ofisi ya TIST, wafanyakazi wa TIST watazidisha kwa malipo ya 4/= ya idadi hiyo ya miti na miche, na kuandaa taarifa kwa vikundi, zitakazorudishwa na **Makwantifaya**. Mpaka sasa vikundi vingi bado vinarudisha mikopo ya mwaka jana, Ofisi ya TIST itaingiza malipo yao ya miti ya kila robo ya mwaka katika **Akaunti** ili kupunguza deni lao lililobakia. Mara baada ya deni kulipwa, kikundi kinaweza kikaanza kupokea fedha.

Vikundi vilivyomaliza kulipa mkopo vinaweza kupewa pesa upya, TIST itaingiza malipo yao katika **akaunti**. Ofisi ya TIST itavijulisha vikundi ni kiasi gani cha pesa iliyopo katika **akaunti**. Vikundi vinaweza kuwaomba Makwantifaya wawaletee pesa wakati wanapokuja kutembelea mwezi unaofuata.

Haya hapa ni mambo matatu ili kuvisaidia vikundi vyenu.

- ◆ Kurudisha mkopo mapema ili kikundi kiweze kupata mkopo upya
- ◆ Kupanda miti mingi kwa sasa na kulipa mapema ili kupata pesa nyingi baadaye.
- ◆ Kuacha pesa katika akaunti ya TIST ili iweze kuongezeka katika muda huo. Kikundi pia kinaweza kununua kitu kama baiskeli au mbegu bora za nafaka, kwa siku zjazo.

Mikutano itakayofanyika kwenye Parishi.

Parishi ziliombwa kuitisha mikutano mara moja kwa kila mwezi, Kwantifaya au wafanyakazi wa Ofisi ya TIST watahudhuria mikutano hiyo. Ni muhimu washiriki wote wa vikundi vidogo vidogo kuhudhuria mikutano hiyo. Yafuatayo yatafanyika katika mikutano ya Parish ya mwezi huu.

- ◆ Kupokea taarifa ya akaunti inayoelezea ni kiasi gani cha pesa kilichopo .
- ◆ Kupokea fedha zilizoombwa na wanakikundi.
- ◆ Kupokea Habari Moto Moto
- ◆ Kwa kuwapatia Kwantifaya taarifa za kila mwezi juu ya mikutano ya vikundi vidogo vidogo.
- ◆ Kuzungumzia maswali yanayohusu mradi.
- ◆ Kushirikishana habari nzuri kutoka katika kazi za vikundi.
- ◆ Kushirikishana njia bora

Vikundi vinawajibu wa kuipatia Ofisi ya TIST taarifa za kila mwezi ili kuweza kupata malipo ya miti. Taarifa hizo hutumika kuisaidia TIST na Dayosisi kwa ujumla itambue ni njia zipi bora katika kuvitumikia vikundi na kuwa mafunzo gani yanahitajika kwa vikundi vidogovidogo.

TIST inafanya kazi kwa jitihada ili iweze kuvisaidia vikundi vidogovidogo. Tafadhali uwe mvumilivu pale

Weekly Meetings for Small Groups are Important!

When you are a member of a Christian small group, having a meeting every week is important for many reasons. The small group gathers to help each other grow spiritually. Small groups are a way for the Body of Christ to gather in love to build each other up into the fullness of Christ, and to receive instruction from the Holy Spirit that benefits the purpose or task of that small group.

Weekly fellowship strengthens you in many ways in your walk with Jesus. You have brothers and sisters in Christ to encourage you, pray with you, help you in difficulty and support you. Bible study gives group members the refreshment of taking in God's word, talking about it with other Christians, and helping each other figure out how to apply it in your lives.

If you are a TIST small group, weekly meetings are also an important time to make plans about your nursery, your tree planting, and your conservation farming techniques. It is a time to discuss njia bora that will benefit other small groups as well as your own. After Bible study, some group members can help each other in weeding or planting.

The small group monthly report forms your small group has received are set up to report on one meeting per week. Giving them to the quantifier at the monthly meeting will help the DMP and TIST know how your group is progressing. You can also put on the form njia bora you have learned and any questions you might have.

KEEP TRANSPLANTING YOUR SEEDLINGS DURING THIS TIME.

Happy New Year to all group members and all people in TIST program. We would like to thank God for the rain.. It is now raining almost everywhere in Mpwapwa Diocese. So we would like to remind all group members that now is the best time for them to transplant their seedlings into the holes. A few months ago we had different seminars about tree planting and conservation farming. Both of these seminars were done in every deanery of Mpwapwa Diocese. Experts from Kenya and Moshi Tanzania (Mr. Alphonse Temu and Mr. Richard Stone-wig) conducted those seminars on tree planting and the conservation Farming seminars

TIST inapojaribu kujifunza mradi huu, zaidi sana uwe mwangalifu na makini ili kuvisaidia vikundi vingi.

Mikutano ya kila wiki ni Muhimu

Wakati unapokuwa ni mwanachama wa kikundi kidogo cha Kikristo, kufanya mikutano ya kila wiki ni muhimu sana kwa sababu mbalimbali. Wanakikundi hucusanyika ilikusaidiana kati ya mtu na mtu kukua kiroho. Kikundi ni njia ya kushiriki mwili wa Kristo pamoja na upendo na kujengana kila mmoja katika kutimiza Ukristo, na kupokea maelekezo kutoka kwa roho mtakatifu ambayo yatanufaisha malengo au matakwa ya kikundi.

Faragha za kila wiki zinakuimarisha katika mambo mengi katika kutembea na Kristo. Unao ndugu katika Kristo wanao kufaraji, kuombea na, kukusaidia katika mambo magumu. Kusoma Biblia huwasaidia wanakikundi katika kufanikisha na kuangalia maneno ya Mungu, kuongea na wakristo wengine, na kusaidiana kila mmoja kufikiri juu ya kuyaendesha Maisha yake.

Kama wewe ni Mwanakikundi wa vikundi vilivyo wanachama wa TIST, Kukutana kila wiki pia ni muhimu sana katika kupanga juu ya vitalu, kupanda miti, na kuwa na mazungumzo juu ya mbinu za kilimo. Huu ni wakati wa kujadili Njia Bora ambazo zitanufaisha vikundi vingine ikiwa ni pamoja na kikundi chako. Baada ya kusoma Biblia, baadhi ya wanakikundi watasaidiana kila mmoja katika kupalilia au kupanda.

Fomu za ripoti ya mwezi mlizopokea kwenye vikundi vyenu zimepangiliwa katika mpangilio wa vikao kwa kila wiki. Fomu mtakazowapatia Kwantifaya katika mikutano yenu, zitaisaidia TIST na Dayosisi ya Mpwapwa kwa ujumla kujua ni jinsi gani vikundi vyenu vinaendelea. Pia mnaweza kujaza Njia Bora mlizojifunza na kuuliza maswali yoyote mliyonayo.

ENDELEA KUPANDIKIZA MICHE YAKO WAKATI HUU

Heri ya mwaka mpya kwa wanavikundi wote na watu wote mliopo kwenye mradi wa TIST. Hatuna budi kumshukuru Mungu kwa mvua ambayo kwa hivi sasa imenyeshwa karibu maeneo yote ya Dayosisi yetu. Hivyo tungependa kuwakumbusha na kusisitiza wanavikundi wote kwamba huu bado ni wakati mzuri kwa watu kuendelea kupandikiza miche yao ya miti kwenye mashimo. Miezi michache iliyopita tulikuwa na semina juu ya upandaji miti na kilimo hai. Semina hizi zote zilifanyika karibu Dinari zote za Dayosisi ya Mpwapwa. Wataalam kutoka Kenya na Moshi Tanzania (ndugu Richard Stonewig na Alphonse Temu) walifanya semina juu ya Upandaji miti. Na

were conducted by LITI trainers (Mr. Msangi, Doberi and Mr. Yibalila).

So please make sure that during Transplanting seedlings and planting maize or millet you follow all required procedures as the experts taught you.

Remember that, to plant at the beginning of the rainy season is much better than planting late. That means your trees will live and become more healthy rather than those planted late which will require you to put water for them to survive.

One point to remind is to remove the plastic tube when transplanting trees and also handling carefully the seedlings when moving them from nursery to the holes. It will be better to take out all the weeds as soon as possible before they become tall. This makes sure nutrients in the soil help the trees, not the weeds. TIST encourages those groups who missed the loan of 2001 program, please keep planting more seedlings in order to have more trees for receiving cash in the new program that is beginning now. Remember as the groups plant more trees that means they will receive more cash.

Another point to remind is that all the groups need to keep record of how many members in the group used the NJIA BORA for Conservation farming. Be free to write that report on the Monthly report forms during your discussion on the weekly meeting. We need that information for future determination whether this method has succeeded or not. When recording names of people who used the Conservation farming do not forget to write how big is the farm to each member.

Now you will have good time in your meeting within your Parish with the Quantifiers, please make sure you give this information including THE small group Monthly report form to the Quantifiers who will bring it to TIST Office.

We hope that you will enjoy participate in the Parish meeting where you will get different ideas from different groups within your Parish and also you will be getting some information from the TIST Office through the Quantifiers.

The TIST office wishes to serve the small group members in as many ways as possible.

semina za Kilimo Hai zilifanywa na wataalamu kutoka LITI (Ndugu Msangi, Dobeli na ndugu Yibalila)

Kwa hiyo hakikisha kwamba wakati wa kuhamisha miche na kupanda mazao mahindi au mtama unafuata hatua zote zilizoelekezwa na wataalam.

Kumbuka kwamba, kupanda mwanzoni mwa msimu wa mvua ni bora zaidi kuliko kuchelewa. Hii inamaan kwamba miti yako itakuwa hai na yenye afya kuliko ile iliyopandwa mwishoni mwa msimu wa mvua ambayo itakuhitaji uimwagilie maji ili iweze kuishi.

Jambo moja la muhimu la kukumbusha ni kwamba wakati wa kupanda miche yako kumbuka kuondoa vinailoni na pia beba miche kwa uangalifu utakapokuwa unatoa miche kutoka kwenye kitalu kwenda kwenye mashimo. Pia litakuwa ni jambo la muhimu endapo mtapalilia magugu yote mapema kabla hayajawa marefu. Hii itahakikisha kuwa virutubisho vya kwenye udongo vitachukuliwa na miti badala ya kuchukuliwa na magugu. TIST inapenda kuvitia moyo vikundi vyote ambavyo havikupata mkopo katika mpango wa mikopo wa mwaka 2001, tafadhali endeleeni kupanda miti sasa ili muweze kuwa na idadi kubwa ya miti ya kupokelea fedha katika mpango mpya unaoanza sasa. Kumbuka kadili kikundi kinavyopanda miti mingi ndivyo kitakavyopokea fedha zaidi.

Jambo lingine la kukumbushana ni kwamba vikundi vyote vinahitaji kurekodi idadi ya wanakikundi waliotumia NJIA BORA katika Kilimo hai. Muwe huru kuandika taarifa hiyo katika fomu za ripoti ya mwezi wakati mnapokutana na kuzungumza katika vikao vyenu vya kila juma. Tunahitaji taarifa hizo kwa tathimini ya baadaye ili kujua kama njia hii imefanikiwa au la! Mtakapoorodhesha majina ya watu wanaotumia njia hiyo, msisahau kuandika pia ukubwa wa shamba la kila mmojawapo.

Hivi sasa mtakuwa na wakati mzuri kufanya mikutano katika Parish zenu mkiwa pamoja na Makwantifaya, tafadhali mnaombwa kuhakikisha kuwa, mnawapatia taarifa hizi pamoja na fomu za taarifa za mwezi Makwantifaya, wao ndio watakoziwakilisha katika Ofisi ya TIST.

Ni matumaini yetu kuwa mtafurahia kuhudhuria katika vikao vyenu vya wanavikundi wote wa Parish mahali ambapo mtapata mawazo tofauti tofauti kutoka sehemu mbalimbali za Parish yenu, na pia mtapata taarifa mbalimbali kutoka katika Ofisi ya TIST kupitia kwa Makwantifaya.

Ofisi ya TIST inapenda kuvihudumia vikundi vidogo vidogo katika mambo mbalimbali kadri iwezekanavyo